

**MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi, Dk.Edmond Mndolwa, akipokea mizinga 700 yenye thamani ya sh. milioni 140 kutoka kwa Mwenyekiti wa Jumuia ya Wazazi Mkoa wa Arusha, Hezron Mbise, kwa ajili ya jumuiya hiyo mkoa wa Arusha, jana. (Picha na Lilian Joel).**

## \*Adhabu yaja atakayepitisha mifugo barabara ya lami\*

**Na FRED ALFRED, Dodoma**

MENEJA wa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijiini (TARURA) Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, John Chaula, ameagiza kuanza kuchukuliwa hatua kwa wananchi watakapitisha mifugo kwenye barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami.

Agizo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki alipokuwa akitoa taarifa ya ujenzi wa barabara za Bahi Mjini kwa kiwango cha lami kwa kamati ya siasa ya mkoa ilipotembelea wilayani hapo.

Chaula, alisema katika kipindi cha kampeni mwaka 2015, wananchi wa Bahi walihidiwa kujengewa barabara kwa kiwango cha lami ambapo hadi sasa jumla ya kilometra 2.3 zimeshajengwa lakini mifugo imeonekana kuwa changamoto katika kuziharibu.

"Serikali imewekeza fedha zake katika

barabara hizi, lazima kila mwananchi azitumie vizuri ili zilete manufaa hata kwa kizazi kijacho ikiwa ni pamoja na kuacha kupitisha mifugo katika barabara hizi kwani ndio chanzo cha kuharibika.

"Mifugo kama ng'ombe na mbuzi ina njia zake tofauti na barabara hizi ambazo serikali imejenga kwa ajili ya wananchi, ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji katika mji wa Bahi," alisema.

Alisema kwa sasa wameandaa sheria zitakazowabana wafugaji kutopitisha mifugo yao kwenye barabara ikiwa ni pamoja na faini kubwa kwa watakaokaidi.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alisema katika kutekeleza miradi yote ya barabara kwa kiwango cha lami, serikali ilitoa kiasi cha sh. bilioni 1.42 kwa ajili ya ujenzi ambapo ulifanyika kwa awamu tatu.

Alisema awamu ya kwanza ni katika

kipindi cha mwaka 2015/2016 kilometra 0.9 zilijengwa kuanza Bahi Mission hadi kilipo Kituo cha Polisi, awamu ya pili mwaka 2016/2017 zilijengwa kilometra 0.7 katika barabara ya Mkuu wa Wilaya.

Mwanahamisi, alisema awamu ya tatu 2018/2019 ilijengwa kilometra 0.7 kwa barabara ya Mwanachungu hadi Bahi sokoni.

### **Miundombinu**

#### **KUPITISHA MIFUGO BARABARANI**

Wakala wa Barabara za Mjini na Vijiini (TARURA) umeagiza kuanza kuchukulia hatua dhidi ya wananchi watakapitisha mifugo kwenye barabara zilizojengwa kwa lami.